



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA



**HOTUBA YA BW. ADAM FIMBO, MKURUGENZI MKUU, TMDA KWENYE  
UTIAJI SAINI WA MKATABA WA MAKUBALIANO BAINA YA HOSPITALI YA  
TAIFA MUHIMBILI (MNH) NA MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA  
(TMDA) KATIKA UKUMBI WA MKURUGENZI MKUU WA MNH – DAR ES  
SALAAM, TAREHE 16/6/2023**

- **Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH),**
- **Watendaji wa Taasisi za MNH na TMDA,**
- **Wageni waalikwa,**
- **Wana Habari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Habari za asubuhi.**

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima, afya na nguvu za kutuwezesha kuwepo hapa leo hii. Pia nitumie fursa hii kuwashukuru nyote kwa kufika kushuhudia utiaji saini wa hati ya makubaliano baina ya taasisi zetu. Hati hii ni kielelezo cha dhamira ya dhati ya pande zote mbili katika kuboresha, kuimarisha na kulinda afya ya jamii.

**Ndugu wageni waalikwa,**

TMDA ni taasisi yenye jukumu la kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa chanjo, dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa za tumbaku. Utekelezaji wa majukumu hayo umekuwa ukifanyika kwa kushirikiana kwa karibu sana na vituo vya kutolea huduma za afya katika kuhakikisha kuwa bidhaa zinazodhibitiwa ni salama kwa matumizi ya binadamu. Hii ni pamoja na



**MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA**

kupokea taarifa za maudhi, madhara au matukio yanayosababishwa na matumizi ya bidhaa za dawa na vifaa tiba.

**Ndugu wageni waalikwa,**

TMDA imekuwa ikitoa elimu pamoja na vitendea kazi katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini ili kuwawezesha watoa huduma za afya kuwasilisha taarifa hizo kwa wakati na kwa usahihi.

Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) imeweza kutumia fursa hiyo na kuwa taasisi inayoongoza kitaifa katika kuwasilisha taarifa za maudhi, madhara au matukio hayo. Hali hii imepelekea kuimarika kwa ushirikiano baina ya taasisi hizi mbili zenye nia moja ya kuboresha utoaji wa huduma za afya na kulinda afya ya jamii.

Takwimu zinaonesha kuwa katika miaka mitatu ya fedha (2020/21,2021/22 na 2022/23), MNH imekuwa ikiongoza kitaifa katika utoaji taarifa wa madhara yatokanayo na matumizi ya dawa kwa kuwa na 57% kati ya taarifa zote zinazopokelewa na TMDA (12,544 kati ya 22,106).

**Ndugu wageni waalikwa,**

Pamoja na ushirikiano huo imeonekana ipo haja ya kuainisha maeneo ya kipaumbele kwa taasisi zote pamoja na kubuni mbinu za kufanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha matumizi ya mazuri ya rasilimali katika utekelezaji wa malengo mkakati ya taasisi zote.

**Ndugu wageni waalikwa,**

Makubaliano haya yanalenga kuimarisha ufuatiliaji wa maudhi, madhara au matukio yatokanayo na matumizi ya bidhaa zinazodhibitwa na TMDA katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ufuatiliaji wa bidhaa za afya katika soko (PMS) na kuwzesha uanzishwaji wa mifumo ya uhakiki



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA



**MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA**

ubora katika idara ya famasi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH). Pia yatawezesha mapambano ya usugu wa dawa dhidi ya vimelea vya magonjwa hivyo kufanikisha malengo ya kuimarisha na kuilinda afya ya jamii.

**Ndugu wageni waalikwa,**

Kwa kuhitimisha, utiaji saini wa mkataba huu ni mwanzo wa safari kuelekea mafanikio ya pamoja na utimilifu wa matarajio yetu. Hivyo tushirikiane bega kwa bega kwa kutumia mkataba huu wa maelewano kama chombo chenye nguvu ya kuleta matokao ya kudumu.

**Asanteni kwa kunisikiliza**